MAHUBIRI N°17: KUKIRI ZAMBI HAZARANI

(*Ilihubiriwa huko Locodjro, Abidjan – Côte d'Ivoire / www.matth25v6.org*)

Angalisho : Vita kubwa ya ujumbe huu haikuwa tu na lengo la kufunua nyoka, udanganyifu, lakini pia kukamilisha kazi ya utakaso wa mwili kama vile wa roho. Na tuko sasa katika jambo la muhimu la mitume: kukiri zambi hazarani. Na hii mafundisho ya hali ya juu ni ya lazima hata kwa zambi ndogo ndogo au zile zinazo tendwa bila kutaka. Kwa mfano, mtu akikuomba pesa nawe unamupa bila kumuuliza swali lolote na yeye anakwenda kuichezea mchezo wa pesa, kununua sigara, pombe,… wala unapo nguruma wala unapo danganyika kuimba wimbo wa kipagani,… wewe ni mwenye makosa. Wala ukijiunga hata dakika moja kuomba pamoja na mtu wa yale makanisa za kikatolika, kiprotestanti, kiinjili au ya kibranhamisti wewe ni mwenyi makosa kama yule anayekwenda kuonana na mchawi au mfumu. Unapo patikana mahali fulani pasipo Biblia na pale kukiwa biblia Louis Segond, au Scofield au Thompson, utatazama yote ile kama mtego. Hamuwezi kutumia misemwa au tamko za mitaani. Iwe kwa ajili ya kifo, wala karamu, wala ndoa, wala kwa ajili ya jambo fulani hamutaingia hata moja ya makanisa yale, makesha yao wala vijiji vyao vya ibada. Ukifanya zambi ndogo kwa mazungumzo pamoja na mtu uliyemjua kuwa mchekeleaji au msengenyaji, ni zambi kubwa kama yule anaye kwenda nyumbani mwa kahaba. Ni zambi ambazo tunalazimishwa kupambana nazo kwani, kwa nukta ambayo tumefikia, yeyote atakaye jiachilia kwa ngono ya upekee, uwongo, uchafu, televisheni, siasa, uzini, wala anaye kosa kutoa zaka au sadaka,... yeye ni kwetu adui wa hatari na yeye ni sababu ya mateso yetu, yeye ni kama mkoma ndani ya kambi ya wana wa Israeli. Kama mtu atatuweka katika masumbuko kama yule Akana wala kufwata ujumbe huu bila kustahili, yeye ni chini ya laana ya 1Kor.11:27-30. Mufanye angalisho kwani zambi siyo asili yetu ya pili. Na Mungu alimwambia Musa: *«Waliyo nijaribu mara kumi hawataingia katika nchi ya ahadi »*. Pia hamupaswi kuungama zambi kwa kicheko midomoni. Kuungama hazarani haipaswe kuwa mahubiri, ushuhuda, kisasi au kujieleza sababu ya zambi lakini kuunguma pamoja na kujuta. Muhepuke maelezo ila tu ikiwa inaombwa na kusanyiko. Kama ulimkosea mtu na huyo angali akizidi kuizungumzia, ni kusema ilimugusa moyoni, hata kama ni kabla ubatizwe, umuombe msamaha na kisha uungame mbele ya kusanyiko. Munaona?

Kama ulikosa, usije kusimama pale na kusema: *"Oh! Wandugu,… Munifahamu!, hata Biblia inasema kwamba mwili ni zaifu, nilifanya kitu fulani… musione ndugu yenu lakini shetani!"*. Si kwako kuwaambia hivi ndugu zako! Uliweza kusema hivi: *"Wandugu, nilimkosea Mungu na nyinyi, nilipatwa na uzaifu, niliwasaliti, sistahili hata kuitwa ndugu! Jambo fulani ilinifikia…"*

Pia, wote walio na mambo ya kuungama waifanye wote na kuwe ombi moja kwa wote kwa kukomboa muda. Juu ya zambi zilizo "zito", neno litapewa kusanyiko kupitia mchungaji wala yule anaye ongoza maungamo hazarani, kwa namna ataongozwa na Roho. Lakini ndugu aliyetubu wala atakaye tubu hastahili kusema juu ya kuungama ya mwingine.

Kuna mambo ambayo haifai ije katika maungamo. Kwa mfano kama haukuweza kusema mbele ya yule anaye jaribu kupinga ujumbe, haitoshi tu kukiri hazarani lakini inakubidi kumwita mtu yule kwa kumwambia yote ile haukuweza kumwambia. Pia, Yule ambaye hakuweza kulipa zaka atatubu tu baada ya kuilipa kama inavyo semwa katika Biblia.

Kama inavyo elezwa katika historia, kutubu sikioni [kuungama mbele ya padre, mchungaji au mbele ya mzee wa kanisa] iliwekwa na wanadamu. Mitume waliweka kuungama hazarani kufwatana na mamlaka walio pewa na Yesu-Kristo mwenyewe katika Yne 20:23. Kuungama hazarani ilivunjwa karibu mwisho wa karne ya III na ikabadilishwa na kuungama sikioni ambayo iliwekwa na mtakatifu Benoît, muundaji wa utaratibu wa wabenedikta lakini haikuwa na ondoleo la zambi. Kwa mwaka 1215, kuungama sikioni ililazimishwa watu kwa mkutano wa Latran na kuifanya kuwa sharti kisha, miaka miwili baadae, kwa mkutano wa Trente, ikageuka sharti isiyoweza kukataliwa. Ni kwa mwaka 758 ndipo kuungama sikioni iliingizwa huko magharibi kwa taratibu za kidini za mashariki na kuchukua nafasi ya kuungama hazarani.

Na nyuma ya kuungama sikioni, padre alikuwa akisema: «*ninakusamehe kadiri ninayo uwezo na pia ginsi unavyo hitaji* ». Badala ya kusema: « *Mungu asamehe zambi zako na zambi zangu pia!* »

Na kwa ushirikiano pamoja na mapadre, wafalme na kaizari wengi walijitwalia faida katika kuungama sikioni kwa kutenda maovu. Mfalme Louis XI aliungama tu wakati alitenda maovu makubwa, na hapo zamiri yake ilikuwa huru. Na aliungama kila mara ijapo, ingalikuwa kuungama hazarani, hangeli fanya hivyo. Na kwa wakati ule kufanya hivi ilikuwa ikikinga utawala wao. Kule Normandie, kijana moja aliungama mbele ya padre akaeleza kwamba alitaka kumwua mfalme François I^{er}. Padre akamuelezea mfalme na ikafwata yale munayojua. Ijapokuwa kama ingalikuwa kwa maungamo hazarani, mfalme hangemfanyia kijana huyo mabaya.

Kuungama zambi mbele ya mtu moja, awe padre au mchungaji haitoke katika Biblia.

Chunguzeni katika historia, na mutaona kwamba katika Israeli, kwa mafungo ya Kippur [msamaha kubwa], kuungama ilikuwa hazarani. Siku ile, wayahudi wote walikusanyika na kuungama zambi zao kama vile tunavyo fanya hapa kwa muda wa 1/4 ya mchana! Siyo robo lakini 1/4 ya mchana, wamoja baada ya wengine… Someni Neh.9:1-3 na mutaona mambo yale ! Munaona? Kumsemea padre au mchungaji zambi zako, ile siyo kuungama lakini ni *siri kati yenu.* Ulimuelezea padre au mchungaji siri yako kwa kutuliza zamiri yako lakini usiseme kwamba ile ni kuungama. Kuungama sikioni au Kuungama ya upekee ni uriti kutoka katolika. Tazama kinachosemwa katika kamusi Littré, kipindi cha 2, ukurasa 633: "*kuungama sikioni au kuungama ya binafsi: kuungama inayo fanyika sikioni mwa padre, kinyume ya kuungama hazarani iliyo fanywa katika Kanisa ya kwanza* ". Tazama yanayo semwa katika Larousse ya karne ya XX, sehemu ya 2, ukurasa 404: "*kuungama sikioni au kuungama ya binafsi: ni ile inayo fanywa katika siri kwa padre [au mchungaji], kuungama hazarani: ni ile iliyo kuwa ikifanyika zamani mbele ya watu* ". musichanganye *kuelezeana siri* na *kuungama*.

[Katika Injili, katika Yne8, mwanamke muzinifu angepaswa kupigwa kwa mawe lakini aliweza kufikia njiapanda ya sheria na neema hapo, neema ilishinda sheria. Munaona? Taifa lote lilitaka kumpiga kwa mawe sawasawa na ile ilikuwa ikifanyika chini ya sheria tangu Musa. Ni Musa aliyo amuru hivi kwani zambi yote ni kinyume cha taifa. Sababu gani wanataka wampige kwa mawe ikiwa hakuwakosea? Munaona? Taifa lote likampiga Akana kwa mawe katika Yosua 7. Zambi ya Akana ikawaletea

matatizo… Musa akawapa mamlaka ya kuua kwa mawe lakini Yesu akatupatia mamlaka ya kusamehe. Munaona? Tunaamini kwamba nyuma ya ubatizo tunaunga mwili moja na hapo zambi ya kiungo moja ni zambi ya mwili mzima. Na Mt.18:18 inasema: *«Kweli, ninawaambia: yote mutakayo funga duniani itafungwa mbinguni, na yote mutakayo fungua duniani itafunguliwa mbinguni»*. Na katika Yoane 20:23, Yesu aliposema: « *kwa yeyote mutakaye ondolea zambi, itaondolewa ;na kwa yeyote mutakayemfungia zambi, itamfungiwa* » ni kwa wanadamu. Munaona? Mara tena, ninakubali Mt.16:19 lakini ni fumbo: mamlaka hayo kwa neema inakuwa kwa mtu moja tu kwa jumla duniani. Ni siri ya Luka 5:20-21 ndio inayo ionyesha. Aliye na funguo ya ufalme [wa mbinguni] ; mtu mmoja ambaye ombi lake linakubaliwa zaidi mbele ya Mungu, linalo nguvu kuliko ombi la dunia zima kwa jumla. Kwa wakati wa mateso, katika 2 wafalme 19, mfalme Ezekia akamtuma Eliakimu, kuhani mkuu, na Shebna, mwandishi, na wazee wa makuhani kwa Isaya, nabii ili apandishe ombi kwa ajili ya Israeli. Wangeweza kusema: « *Ee mfalme, tunakwambia kwamba tulipanga mafungo Yosafati kwa nchi yote kwa jumla na mafungo Esiteri imeandaliwa na hapo tumekubaliwa na makanisa zote kwa jumla na maprezidenti wao hata manabii mia nane waliona mbeleni kwamba itafaulu* ». lakini mfalme alisema: nendeni kwa Isaya, nabii aliye peke juu yetu sisi wote! [*Kusanyiko linasema*: *Amina*!]

Lakini pia, kuungama hazarani ni jambo mbaya kwa watumishi wa zambi katika makusanyiko. Ndio maana hawaitaki! Wanahuzunika kuungama hazarani inapotajwa. Mtu wa kusanyiko la miungu aliniambia: *"Ujumbe ni ya kweli na sasa napenda nije lakini… hasa kama uliondoa kuungama hazarani, ungelipata watu wengi!"* wengine wanasema: " Kama mtu anaungama hazarani, wengine watakwenda kuizungumzia nje!" Wandugu, kama ni hivi, musifanye basi zambi! Kuhusu kuungama hazarani, Yobu anasema nini? Tuisome, Yobu 31:33-34: « *kama nilifunika kosa langu kama Adamu, kwa kuficha uzalimu wangu katika tumbo langu, kwa sababu niliogopa kundi kubwa, na kwamba niliogopa kuzarauliwa na jamaa, na nikabaki kimya…* » mustari wa 40: « *…miiba zikomae badala ya ngano, na magugu pahali pa shayiri*! » Munaona? Yobu anasema kwamba kama, kwa ajili ya kundi la watu, kwa ajili ya kuzaliwa na watu, alificha zambi yake moyoni mwake, anapo fanya mpango, mpango ile ishindwe! Kama ulipata nguvu ya kufanya zambi na tena unapata haya au woga kwa kuiungama hazarani kama Yobu, hapo sasa laana ni juu yako na juu ya yote utakayoiwekea mkono!

[*Ndl: Tangu tarehe 03 januari 2006, ndugu Filipo anakaa mtaa wa Abobo, karibu na kusanyiko iliyo kazi ya ndugu Bitty. Lakini tarehe 22 januari 2006, ndugu Filipo alikuja kuhubiri katika kusanyiko la Lokodjro kuhusu hali moja ya uchafu iliyo ungamwa na ndugu moja tarehe 08 januari na iliyo pinganisha kusanyiko zima na ndugu Arsene aliye shikilia peke kwamba ndugu yule hapaswe kuombewa. Na ndugu Filipo alishikilia msimamo wa ndugu Arsene alipo sikia mambo yale. Mahubiri yale yanapatikana kwenyi kaseti. Tazama sehemu moja …*].

Niliumwa sana kuona kwamba japo kupinga ya ndugu Arsene, mulimuombea ndugu aliye ungama! Ninahukumu tendo hilo la demokrasia. Kama kutoka kwangu huko Locodjro ingalikuwa kifo, ujumbe huu ungalikuwa je mikononi mwenu? Ninyi mulio wakati wote kisimani kwa muda wa miaka tatu na mulipaswa kuwa kielelezo kwa kusanyiko zingine? Kwa hiyo, wandugu, mulitenda vibaya!...

Kuhusu matokeo ya watu nyuma ya kuungama hazarani, sisi si katika chumba cha shule na hatutaki wachunguzi wasujaa wa maungamo, watu wanao sukumwa kujieleza kwa kila ungamo… kuhusu kusamehe, kusanyiko ni huru kusamehe au kukataa kusamehe kwa mamlaka iliyo pewa kwa Kanisa na Mungu katika Mt.18:18 na Yne.20:22. Mtu asiseme: *"Sisi wote ni watenda zambi; basi inatubidi kusamehe"*. Katika Agano la Kale, ni wanadamu kama sisi walio pewa na Mungu mamlaka ya kupiga kwa mawe. Hatupaswe kufanya hesabu wala kuangalia uzaifu wetu kwa kuweka Neno kazini. Hatuna ruhusa ya kuvunja Neno kufwatana na sisi wenyewe! Na kama ndugu asiye na heshima kwetu na kwa Ujumbe anakwenda kutenda zambi ya ngono, ninaomba miezi mitatu kisha kuungama aje na msichana kabla aombewe na ni utaratibu… [Ndl: Ndugu mmoja anasema: *"Na kama basi msichana hataki kuja?"*]. Atakuja! Kwa nini hatakuja? Jinsi, ndugu huyu alikuwa mwenye hekima kwa kumpeleka katika hoteli, atakuwa pia mwenyi hekima kumleta hapa. Na kama alikubali kwenda katika hoteli ili aondolewe mavazi, siyo katika hekalu ndipo atakataa kuja! Yeye ana jukumu ya kumleta hapa ili tuone kwamba hana mimba na tena kwamba hakuna shida lingine kabla ya kumuombea, ikiwa ataombewa. Na kusanyiko itaamua kama anaweza kuja kuhuzuria ibada au hapana, kwa muda wa miezi hiyo mitatu. Kwa sababu zambi ya ngono haifike kwa ghafla, ndugu au dada ataleta sababu ya tendo lake. Munaona? Lakini ikiwa hali ya uzinifu, ndugu au dada atakwenda kwanza kuungama kwa wale mke na mume wengine pamoja na washuhuda wawili. Kama ndugu ana mke au dada ana mume, ataungama kwanza kwa mke au mume wake kisha atasindikizwa na mshuhuda moja zaidi ya mke au mume wake kwa kuwakwendea wale mke na mume wengine. Ni nyuma ya mwenendo hii ndipo ataungama mbele ya kusanyiko… Siyo kwa sababu sisi tuna nguvu lakini pamoja na msaada na neema ya Mungu, kama Yosua na Kalebu tunasema kwa imani kwamba tunaweza! Amina! Tumsifu tu! Tuimbe na tusifu jina lake! [Kusanyiko inaimba: *Wakati ningali hai duniani ; nitasifu jina lako*].

1°. Wakati ningali hai duniani ; nitasifu jina lako.
Kwako utukufu, kwako sifa zangu;
Ee Mungu wa [Musa / Yoshua], nitasifu jina lako.

2°. Wakati ningali hai duniani ; nitasifu jina lako.
Kwako utukufu, kwako sifa zangu;
Ee Mungu wa [Elia / Elisa], nitasifu jina lako.

3°. Wakati ningali hai duniani ; nitasifu jina lako.
Kwako utukufu, kwako sifa zangu;
Ee Mungu wa [Branham / Filipo], nitasifu jina lako.

MAWASILIANO: Ndugu Filipo:+ 225-0252-0252 E-mail: kacou.philippe@yahoo.fr
Upate mahubiri katika site ya: www.matth25v6.org